

193

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOMBERO

KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA KUGAWA
ARDHI WILAYA KILICHOFANYIKA TAREHE 07/06/2010 KATIKA UKUMBI WA
MIKUTANO BOMANI/IFAKARA

WALIOHUDHURIA:

1. Bwana F. Malembeka	-Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya	-Mwenyekiti
2. Bwana J.H. Nzyela	-Afisa Ardhi Mteule wa Wilaya	-Katibu
3. Ndugu S.V. Mdalahela	-Afisa Mipango Miji	-Mjumbe
4. Mh. F. Mgoli	-Diwani Kata ya Mbingu	-Mjumbe
5. Mh. H.L. Mbalahami	-Diwani Kata ya Ifakara	-Mjumbe
6. Ndugu V. Kunambi	-Kaimu Mhandisi wa Ujenzi wa Wilaya	-Mjumbe
7. Bi. Kitua M.J.	-Afisa Kilimo/Mifugo wa Wilaya	-Mjumbe
8. Ndugu J. Simlongele	-Kaimu Mpima Ardhi Kiongozi	-Mjumbe
9. Ndugu O.O. Mpombo	-Afisa Ardhi Msaidizi	-Mwandishi

AGENDA ZILIZOJADILIWA:

1. Ku fungua kikao
2. Kujadili maombi ya ardhi kutoka Kampuni ya Green Resources Ltd katika Vijiji vya Uchindile, Kitete na Taweta.
3. Kufunga kikao.

MUHTASARI NA. 01/06/2010 – KUFUNGUA KIKAO:

Mwenyekiti kabla ya kufungua kikao aliwaomba radhi wajumbe kwa kutofanyika kikao tarehe 01/06/2010 kwa sababu ya kutokamilika kwa mawasiliano. Aliongeza kusema kuwa masuala ya ardhi ni nyeti sana na kwa hiyo yanahitaji kuwa makini wakati wa kujadili.

Baada ya kusema hayo Mwenyekiti alifungua kikao saa 6.00 mchanai.

MUHTASARI NA. 02/06/2010 – KUJADILI MAOMBI YA ARDHI KUTOKA KAMPUNI YA GREEN RESOURCES LTD

Katibu aliwasilisha maombi kutoka Kampuni ya Green Resources Ltd ambayo iliomba ardhi kutoka katika vijiji vya Uchindile hekta 14,682, Kitete hekta 10,555 na Taweta hekta 50,000.00

Maombi yote yalipokelewa na kujadiliwa kama ifuatavyo:-

Maombi ya hekta 14,682 kutoka Kijiji cha Uchindile

Kabla mjumbe mmoja hajatoa maoni yake alitaka kujua miliki itakayotolewa ni ya muda gani.

Afisa Ardhi Wilaya alijibu kuwa ni miliki ya miaka tisini na tisa (99). Baada ya jibu hilo mjumbe alitahadharisha kuwa kama ardhi itaendelea kutolewa kwa mtindo huo wananchi wengi watakosa ardhi siku zijazo.

Afisa Mipango Miji na vijiji alitatoa wasi wasi wajumbe wa kikao kuwa eneo linalotolewa ni lile lisilofaa kwa kilimo na halitumiki kabisa na kijiji lakini linafaa kwa kupanda miti.

Kwa mujibu wa mawasilisho ya Katibu, eneo lililoombwa sehemu moja ni ombi jipya na sehemu nyingine ni fidia ya kipande cha ardhi (hekta 5,474) ambacho kampuni ilikuwa imemilikishwa kinachoangukia katika msitu wa Serikali katika Wilaya ya Mufindi.

Maombi ya hekta 10,555 katika Kijiji cha Kitete

Eneo lililotolewa kwa wawekezaji ambalo ni asilimia arobaini na nane (48%) ya eneo lote la kijiji lilionekana kwa wajumbe kuwa ni kubwa mno. Kutokana na hilo, wajumbe walishauri kampuni nyingine itakayoomba ardhi isipewe. Aidha, walishauri elimu ya ardhi itolewe kwa wananchi.

Mjumbe mmoja alitoa taarifa kuwa eneo lililotolewa ni la mlimani ambalo wananchi huwa hawalitumii kwa kilimo. Hata hivyo hoja hiyo ilionekana haina uzito baada ya mjumbe mwingine kueleza kuwa maeneo ya milimani yanaweza kutumika kwa kilimo kama utaalam sahihi utatumika.

Ilitolewa taarifa kuwa kampuni ina mpango wa kutoa ushuru utakaotokana na hewa ukaa kwa vijiji vyenye mradi wa miti na kwa Halmashauri ya Wilaya. Ilishauriwa kuwa ni vema mikataba ikaandaliwa kwa ajili ya kupata ushuru huo.

Maombi ya ardhi hekta 50,000 kutoka Kijiji cha Taweta

Kwa mujibu wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji hicho, kijiji kina eneo la hekta 47,733.73. Hii ndiyo kusema kiasi cha ardhi iliyooombwa na kampuni hakiwezi kupatikana.

Kwa kuwa Muhtasari wa Kijiji uliandaliwa mwaka 2005 wajumbe walisema mambo mengi yatakuwa yamebadilika. Kwa hiyo ilishauriwa maombi hayo yakajadiliwe upya kwa kuzingatia Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi.

Baada ya kujadili kwa kirefu kulikuwa na maazimio kama ifuatavyo:-

Maazimio:

1. Kwa kauli moja kamati ilipitisha ardhi hekta 10,555 zilizoombwa kutoka Kijiji cha Kitete, na hekta 14,682 zilizoombwa kutoka Kijiji cha Uchindile.

Maombi ya hekta 50,000 kutoka Kijiji cha Taweta yalirejeshwa yakafanywe upya kwa kuzingatia Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi.

2. Kampuni ya Green Resources Ltd ijenge masijala ya Ardhi kwenye kila kijiji kilichotoa ardhi yake ili wananchi wake nao wapate faida zitokanazo na hati miliki.



IDENTIFY THAT THIS IS A
TRUE COPY OF THE ORIGINAL

MUHTASARI NA. 04/06/2010 – KUFUNGA KIKAO:

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango ya mawazo na alifunga kikao saa 7.20 mchana.

UMETHIBITISHWA:

Jina: FIKIRI MALIMBEKA Jina: JOHN NZYELA

Cheo: MWENYEKITI Cheo: IKATI BU
AFISA ARDHI MTEULE (W)

Sahihi: [Signature] Sahihi: [Signature]
MKURUGENZI KILOMBERO

MALMASHAURI YA WILAYA KILOMBERO
Tarehe: P.263 IFAKARA, KILOMBERO Tarehe: 16-06-2010
16-06-2010

ICERTIFY THAT THIS IS A
TRUE COPY OF THE ORIGINAL

